**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI MRADI WA MAJI WA MJI WA ORKESUMET WILAYA YA SIMANJIRO, MKOANI MANYARA

**TAREHE 15 MACHI, 2022**

***Mheshimiwa Juma Aweso (Mb), Waziri wa Maji;***

***Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri mliopo;***

***Mheshimiwa Makongoro Nyerere, Mkuu wa Mkoa wa Manyara;***

***Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Manyara na Arusha;***

***Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu Wizara ya maji,***

***Ndugu, Caroline Mthapula, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Mkoa wa Manyara;***

***Katibu Tawala wa Wilaya zote za Mkoa wa Manyara;***

***Wawakilishi kutoka Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA);***

***Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazozalisha mafuta (Opec Fund for International Development -OFID);***

***Wakurugenzi na wenyeviti wa Halmashauri za Mkoa wa Manyara;***

***Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi wa Bodi za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira;***

***Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Manyara;***

***Wakuu wa Taasisi za Serikali mliopo;***

***Viongozi wa Serikali na Chama mliopo;***

***Viongozi wa Dini;***

***Watumishi wa Wizara ya maji na taasisi zake mliopo;***

***Wakandarasi na Wahandisi Washauri;***

***Waandishi wa Habari;***

***Wageni Waalikwa;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....!***

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, afya na kutuwezesha kukutana mahali hapa katika hafla hii ya uzinduzi wa wiki ya maji ambayo inaambatana na uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa maji wa Orkesumet hapa Wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara.

**Pili**, nitumie fursa hii pia kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Manyara hususan wakazi wa Simanjiro na Viongozi wote wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa ndugu yangu Makongoro Nyerere, kwa mapokezi mazuri mliyonipa mimi na ujumbe wangu tangu nilipowasili katika Mkoa huu. Nawaletea Salamu za upendo kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais amenituma niwaeleze kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita anayoiongoza inatambua changamoto zinazowakabili na anaomba ushirikiano wenu ili kwa pamoja tuweze kuzitatua changamoto hizo.

**Tatu**, kipekee kabisa nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge na Waziri wa Maji pamoja na uongozi mzima wa Wizara ya Maji kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika hafla hii muhimu ya kuzindua Wiki ya Maji ambayo itahitimishwa tarehe 22 Machi siku ambayo Dunia nzima itaadhimisha Siku ya Maji Duniani.

***Ndugu Viongozi na Wananchi wenzangu,***

Sote tunafahamu kuwa maji ni miongoni mwa mambo muhimu yanayogusa maisha ya kila kiumbe katika sayari hii ya dunia. Kwa kutambua hilo, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2020 imelenga kila mwananchi kupata huduma ya majisafi na salama, kwa vijijini **asilimia 85** na mijini **asilimia 95** kufikia mwaka 2025. Ili kuweza kufikia malengo haya, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia imetoa kipaumbele cha juu kugharamia miradi mikubwa ya maji. Aidha, Serikali pia imeendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuimarisha sekta hii ya maji ikiwa ni pamoja na kuendelea kulinda na kutunza vyanzo vya maji kupitia Bodi za Maji na Mabonde. Vilevile, Serikali imeendelea kukarabati na kujenga miundombinu mipya ya usambazaji maji; pamoja na kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya kusimamia sekta ya maji ikiwa ni pamoja na kuanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency - RUWASA*).

***Ndugu Wananchi Wenzangu,***

Kaulimbiu ya Maadhimisho ya Wiki hii ya Maji inasema "***Maji Chini ya Ardhi; Hazina Isiyoonekana kwa Maendeleo Endelevu***". Nafahamu Kaulimbiu hii imetokana na Kaulimbiu ya mwaka huu ya Siku ya Maji Duniani inayosema **"G*roundwater: making the invisible visible*",** ambayo kwa tafsiri rahisi ya

Kiswahili ni "***Maji chini ya Ardhi**: **Wezesha kisichoonekana kionekane***". Msisitizo katika kaulimbiu hizi ni umuhimu wa Maji chini ya Ardhi. Wengi wetu hatutilii maanani uwepo wa maji chini ya ardhi kama moja ya rasilimali muhimu sana. Kwa mujibu wa takwimu za Kituo cha Kimataifa cha Tathmini ya Rasilimali za Maji ya Chini Ardhi (*International Groundwater Resources Assessment Centre*), Maji Chini ya Ardhi pamoja na matumizi mengine, hutoa karibu nusu ya maji yote ya kunywa duniani. Vilevile, karibu asilimia 40 ya maji ya chini ya ardhi hutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji; na moja ya tatu ya maji yanayohitajika viwandani hutoka chini ya ardhi. Hii inaonesha kuwa maji chini ya ardhi ni hazina muhimu na yenye thamani kubwa sana kwa maendeleo endelevu ya jamii zetu!

Kwa kutambua hili, ndio maana Serikali kila mara inawakumbusha na kuwasisitiza kuhusu Uhifadhi wa Mazingira na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwani ni msingi wa uendelevu wa upatikanaji wa maji. Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na uchafuzi wa vyanzo vya maji na uharibifu wake unaotokana na shughuli za kibinadamu zikiwemo ukataji miti hovyo, uchomaji wa moto huchangia kupungua kwa rasilimali za maji na hivyo kusababisha ukame na hatimaye ukosefu wa maji kwa matumizi ya binadamu na shughuli za maendeleo kama kilimo na ufugaji. Sote hapa ni mashahidi katika Wilaya hii ya Simanjiro, kipindi cha kiangazi kilichomalizika hivi karibuni tulishuhudia mifugo zaidi ya elfu sitini imekufa kutokana na kukosa maji pamoja na malisho. Lakini pia nitumie fursa hii kusisitiza na kuwasihi tushirikiane kuyatunza mazingira yetu ili tuepukane na majanga haya. Mkuu wa Mkoa pamoja na viongozi wote, hatuna budi kuwa wakali kwenye suala zima la utunzaji wa mazingira. Lazima zifanyike juhudi za ziada katika kupanda miti ambayo ni rafiki kwa mazingira na kusimamia usafi wa mazingira yetu kwa ujumla. Kila Halmashauri ihakikishe inakuwa na Idara ya Mazingira yenye watumishi wenye weledi wa kutosha katika masuala ya mazingira na Idara hizo zipewe bajeti ya kutosha katika kutekeleza majukumu yao. Wakurugenzi wote tekelezeni hili.

Napenda nirejee msisitizo nilioutoa siku ya kuzindua Sera ya Mazingira kwamba kazi ya kuhifadhi mazingira ikiwemo kulinda vyanzo vya maji, misitu, upandaji miti, kupendezesha miji yetu kuanzia sasa lazima iwe ya kudumu.

***Ndugu wananchi,***

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2019, jumla ya miradi ya maji 1,423 imetekelezwa, ikiwemo miradi ya maji 1,268 ya vijijini na miradi 155 ya mijini.

Hii inahusisha miradi mikubwa na ya kimkakati katika miji ya Arusha, Kigoma, Lindi, Same, Mwanga na huu wa Orkusemet hapa Mkoani Manyara. Aidha, tangu mwaka 2020 hadi hivi sasa, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya maji vijijini kwa kuwa na miradi ya kukarabati na kupanua miundombinu iliyopo na kutekeleza miradi mipya.

Hivi punde tu nimetoka kuweka jiwe la msingi kwenye Mradi wa Maji wa Ruvu Remit, uliopo hapa Orkesumet, Simanjiro. Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu kwa Nchi za Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (OFID) kupitia mkopo wa masharti nafuu. Kama ambavyo mmesikia katika taarifa iliyotolewa, mradi huu wa maji ni mkubwa na umejengwa kwa gharama kubwa ya TZS Bilioni 41.51. Aidha, Mradi huu unakadiriwa kukidhi mahitaji ya maji kwa miaka ishirini ijayo kwani una uwezo wa kuzalisha takribani lita milioni 6.72 kwa siku dhidi ya mahitaji ya sasa ambayo ni lita milioni 1.5 kwa siku. Nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wetu wa maendeleo kwa kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa mradi huu muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Aidha, nafahamu kuwa bado kuna baadhi ya vijiji na maeneo mengine ya karibu bado hayajapata maji. Hivyo, naelekeza Wizara ya Maji, Mkoa na Halmashauri ziongeze juhudi za kupeleka maji kwenye maeneo hayo ili wananchi wengi zaidi wafaidike na huduma hii ya maji. Vilevile, mtafute namna ya kuongeza majosho ya kunyweshea mifugo ili wanachi hawa wasitembee umbali mrefu kwenda kutafuta maji ya mifugo yao.

***Ndugu zangu;***

Mradi huu wa maji hapa Orkusemet ambao nimeuzindua leo pamoja na miradi mingine mingi ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo katika Ibara ya 97 inatambua kuwa maji ni msingi wa uhai wa binadamu na ni injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Nichukue fursa hii kumpongeza, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuzidi kutilia mkazo huduma hii muhimu kwa maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi. Aidha, nimpongeze pia Waziri wa Maji na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya kuendeleza mipango ya kuongeza upatikanaji wa huduma za maji katika maeneo ya vijijini na mijini. Na pia niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Simanjiro waliohusika kwa namna moja ama nyingine katika hatua zote za ujenzi wa mradi huu na hasa wale ambao walilazimika kupisha njia za miundombinu ya mradi.

Sambamba na pongezi hizi, nitoe wito pia kwa Viongozi wa Halmashauri ya Simanjiro na Mkoa wa Manyara, kuendeleza juhudi hizi za Serikali kwa kusimamia vema na kuutunza mradi huu wa maji pamoja na miradi mingine yote ya maendeleo katika Halmashauri yetu ya Simanjiro. Aidha nitoe onyo, Serikali itachukua hatua kali dhidi ya kiongozi atakayefanya uzembe katika utekelezaji wa mradi huu na pia wananchi watakaohusika na uharibifu wa mradi huu hatutasita kuwachukulia hatua stahiki. Kila mmoja wetu akawe mlinzi wa hii miundombinu.

***Ndugu Wananchi Wenzangu;***

Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia itaendelea kujenga miradi mbalimbali ya huduma za kijamii ikiwemo ya maji nchi nzima ili kukabiliana na changamoto za maji kwani upatikanaji wa uhakika wa huduma ya maji safi na salama, pamoja na usafi wa mazingira, huchangia sana katika kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.

Aidha, nitoe rai pia kwa Mamlaka za Maji pamoja na wadau wengine wa sekta ya maji kuongeza weledi katika usimamizi wa rasilimali za maji; kujenga miundombinu mingi zaidi ya kutunza maji na kuvuna maji ya mvua, kama vile mabwawa; kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji, hususani kwenye kilimo; na kutunza vyanzo vya maji kikiwemo chanzo cha maji ya mradi huu (Mto Ruvu - Pangani)/Bonde la mto Pangani ili vyanzo hivi viwe endelevu.

Ninaamini tunapozindua wiki ya maji na mwisho kuadhimisha Siku ya Maji Duniani tutaendelea kuelimishana kuhusu umuhimu wa maji ya chini ya ardhi na hivyo kuongeza ufahamu juu ya rasilimali hii isiyoonekana. Natarajia kupitia wiki hii, mtaboresha ubadilishanaji wa maarifa na ushirikiano ili tuweze kutunza maji yetu ya chini ya ardhi na hivyo kuchochea maendeleo endelevu.

*Baada ya maneno hayo, sasa* ***natamka rasmi kuwa Maadhimisho ya Wiki ya Maji 2022 yamezinduliwa rasmi****.*

**Mungu ibariki Afrika**
**Mungu ibariki Tanzania**
**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**